Nimefurahi kukukaribishwa kuwa mgeni rasmi leo. Pia nimefurahi kwamba mahafali haya ni baada ya mitihani. Sioni pointi ya mahafali kufanyika kabla ya mitihani, kwa hiyo nimefurahi kuona wanaongoza shule hii wana busara. Ndiyo nimeona shule hii inaongozwa kwa busara.

Mwalimu mkuu wa shule hii Marimeni ni mama mzuri. Tumefanya kazi naye kwa muda tu lakini ni mama na mwalimu mwenye lengo la kusaidia shule yake na wanfunzi wake. Sio kama ana mawazo tu, anaonyesha kuwa na nguvu ya kutosha kutafsiri mawazo kuwa matokeo, na pia kwa sababu yuko tayari kwenda polepole na utaratibu na kuwa mvumilivu.

Nafikiri mwalimu kama huyu ni mfano mzuri kwa wanafunzi wake – hasa kwa wasichana kupewa kioo kuona ukiwa na malengo, na ukiweza kuanza polepole na kuwa na lengo kuwa mshindi utashinda.

Natumaini wanafunzi wengi wameandika mitihani ya darasa la saba vizuri na kwamba watafaulu na kwenda sekondari. Hata kama hawatafaulu wakisoma ufundi ni vizuri tu. Kitu cha muhimu ni kuendelea na elimu.

Mkimaliza darasa la saba na mkifikiri ni mwisho wa shule na kwa hiyo ni mwisho wa elimu naona mtapata shida katika maisha yenu.

Naomba nyinyi wanafunzi mnaopata mahafali leo kwamba leo unasherekisha kumaliza hatua tu au kiwango. Hii ni hatua ya kwanza ya kujenga maisha yenu. Sio watoto sasa ni vijana, na vijana mna madaraka kuwa mfano mzuri kwa wadogo zenu.

Kama mwalimu mkuu hapa, na natumaini walimu wenu wengine, wamekuwa mifano katika maisha yenu mpaka sasa, na sasa ni zamu yenu kuwa vioo kwa wadogo zenu – nyumbani, kijijini, barabani na popote mnendapo.

Watu wazima wanapenda kulalamika kuhusu adabu ya vijana, na mara kwa mara wana haki kulalamika.

Siku hizi kuna hatari katika maisha, lakini bado vijana wengi wanafikiri sio muhimu kujitunza sio muhimu kupanga, na sio muhimu kutii mamlaka ya jamii.

Kuna shida: shida ya wasichana kuwa wajaa wazito; shida ya wavulana kuvuta sigara na kuvuta bangi; kuna shida ya wote kuhusu HIV/Aids ukimwi.

Wasichana, nimeona wengi wanaharaka kuwa mama. Wanaona nikipata mume na mtoto basi nitaitwa Mama Emma au Mama Beatrice na nitaonakana kama nimefika. Lakini fikirieni tena – nimeona wasichana wengi kufanya haraka na mwisho wanabaki nyumbani bila pesa na maisha magumu mno, na kweli ni kama housegirl bila hata mshahara. Nani anataka kuwa housegirl – na nani anataka kuwa housegirl bila mshihara? Kama jibu ni Hapana, basi nakuombeni kutokufanya haraka na kupanga maisha. Soma

kwanza kwa nguvu, pata kazi na halafu panga utaratibu kupata mume na watoto. Maisha ni marefu – hakuna haja kufanya haraka – onja kila kitu polepole na usiwe mjinga kula kwa pupa.

Wavulana – nimeona wengi wanaoona pesa ni muhimu tu. Wanafikiri wakiacha shule na wakipata kazi mlimani watapata pesa nyingi na wataweza kuringa vizuri. Lakini nimeona wengi wanapanda mlima kwa shida, wamepewa bangi kuwapa nguvu – na wanaanza kutumia pesa zote kwa ajili ya bangi, pombe na sigara. Kuringa kuko wapi? Ni ujinga kabisa, na ni njia ya kuharibu vizuri maisha. Maisha ni marefu – hakuna haja kufanya haraka. Soma kwanza kwa nguvu, pata kazi na halafu panga utaratibu kujenga nyumba na kupanga familia.

Kwa nyinyi nyote nataka kuongea kidogo tu kuhusu ukimwi. Siku hizi ugonjwa wa ukimwi unathiri watu wengi na hasa vijana, lakini hakuna haja kupata ukiwa mwangilifu.

Ukifanya mapenzi uko hatarini ya kupata ukimwi. Ukifanya mapenzi kwa siri majanini au popote basi hakuna mtu anayeweza kufahamu na kwa hiyo ni juu yako kabisa kujitunza.

Je, ungekwenda kununua litre moja ya petroli na kunywa? Ukikunywa kuna nafasi ya kuweza kufa lakini kwa hakika utakuwa mgonjwa kabisa. Sawa, nafikiri usingali nunua petroli na kunywa. Basi, usifanye mapenzi au usifanye mapenzi bila ya kutumia kondom

vinginevyo ni kama kunywa petroli – unaweza kuwa mgonjwa na hata kufa. Pia kwa wasichana kuwa na nafasi ya kuwa mjaa mzito – na hii italeta shida nyingine nyingi.

Kwa hiyo nyinyi nyote mnaingia sasa hatua ya pili kujenga maisha yenu na hatua hii ni muhimu kuliko zote. Hakuna walimu kukuongozeni kama mlivyoongozwa hapa shuleni Marimeni. Nyinyi ni vijana na mnapaswa kuchukua madaraka kwa maendeleo yenu. Nakuombeni kutumia busara na  kufahamu hakuna haraka katika maisha yenu, na ukijaribu kujenga maisha yako kwa haraka hayatakuwa mazuri. Sasa hatua hii nyingine ni kujenga msingi. Hapa Marimeni pamoja na walimu wenu mmechimba msingi. Sasa mpo ndani ya msingi na ni juu yenu kuamua sasa kujenga msingi wa maisha yenu kwa mawe kuwa imara, na udongo au mchanga kuwa sawa lakini kukosa nguvu au kubaki na shimo hilo ambalo mmechimba na mmeandaa hapa Marimeni na walimu wenu. Kila mtu atakushauri kuweka mawe. Lakini sio kupata lori moja ya mawa na kutupa tu – hapana, ni kuweka kila jiwe utaratibu kwa msingi kuwa na pima maji. Kwa hiyo ni kusoma sekondari au ufundi kwa bidii, kuendelea kuishi vizuri na wazazi na kuwatii, kuishi vizuri kijijini kuheshima wazee na kusaidia wadogo, kuvaa vizuri na sio makusudi kushangazi watu, na kuongea vizuri na sio kutumia maneno machafu. Muhimu pia ni kutokushawishiwa na wenzako kufanya vitu vibaya. Simama imara na kanuni, na utaheshimiwa.

Fikiria sasa kuhusu mtu kijijini kwako ambaye ni maskini, hana marafiki wengi, haheshimiwi, na hana maisha mazuri. Sasa jiulize kama mwishoni unataka kuwa kama yeye? Kama hutaki – basi sasa fahamu unaingia hatua kuumba maisha yako na ni uamuzi

wako kuwa mwishoni kama yeye au hapana, lakini unachagua njia sasa. Ukichagua njia ambayo sio sawasawa ni ngumu mno kubadilisha. Chagua vizuri sasa.

Basi nakutakieni maisha mwema, na narudia msikimbilieni kuonja kila kitu kwa haraka – maisha ni marefu na waombeni kuendelea polepole.

Asanteni sana.